

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA

16 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 16 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

332. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, tangu kuanzishwa kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni kiasi gani cha fedha kimewekezwa na nini faida na hasara za uwekezaji huo.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

333. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, mashine ngapi za kukusanya mapato zilibainika kutokuwa hewani na kutotambulika na Halmashauri 2018/2019 hadi 2020/2021.

334. MHESHIMIWA GEOFFREY IDELPHONCE MWAMBE (MASASI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itasimika taa katika barabara za mitaa Mji wa Masasi ili kuongeza usalama na kuhamasisha shughuli za biashara.

WIZARA YA KILIMO:

335. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaruhusu bei ya zao la Kahawa kuamuliwa na nguvu ya soko.

336. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo kuchimba visima virefu katika Bonde la Dominiki Kata ya Mwangeza.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

337. MHESHIMIWA KASSIM HASSAN HAJI (MWANAKWEREKWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni haja ya kubadili utaratibu wa malipo kwa Wastaafu wa Jeshi la Polisi wa Zanzibar ili kuondoa usumbufu wanaoupata.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

338. MHESHIMIWA MARIAM MADALU NYOKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga barabara ya Mletele – Msamala - Mkuzo hadi Namanditi kwa kiwango cha lami.

339. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa barabara ya Dodoma – Iringa katika Mlima Nyang'oro.

340. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Barabara ya Kibaoni - Majimoto hadi Inyonga kwa kiwango cha lami.

341. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga vivuko ili kuweza kupita magari, pikipiki na baiskeli katika reli ya Bandari ya Isaka - Msalala.

WIZARA YA NISHATI:

342. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya wateja waliolipia Shilingi 27,000/= ambao wanatakiwa kulipa fedha zaidi ili kuunganishiwa umeme.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

343. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaondoa Kijiji cha Ngaresero kwenye eneo la Pori Tengefu la Pololeti baada ya kujumuishwa kimakosa.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

344. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha Uwanja wa Ushirika Moshi ili kukuza utalii wa michezo nchini.

WIZARA YA MAJI:

345. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka Mradi wa Maji katika Kijiji cha Nkundi - Nkasi Kusini.

346. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini ahadi ya kupeleka Mradi mkubwa wa maji Tunduma itatekelezwa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

DODOMA
16 MEI, 2023

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE

